Ulimwengu Huu Siyo Kwetu

na

Ellis P. Forsman

Ulimwengu Huu Siyo Kwetu

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Ulimwengu Huu Siyo Kwetu

Fil. 3:20-21

Fil. 3:20-21, "*Kwa maana sisi wenyeji wetu uko mbinguni, kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo; atakaye ubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uwezo ule ambao kwa huo uweza hata kuvitiisha vitu vyote view chini yake.*"

Yakobo anaelezea maisha yake kama usafiri.

Mwanzo 47:9, "*Yakobo akamjibu Farao, siku za miaka ya kusafiri kwangu ni mia na thelathini, siku za miaka ya maisha yangu zimekuwa chache, tena za taabu, wala hazikufikilia siku za miaka ya maisha ya baba zangu katika siku za kusafiri kwao.*"

Kulingana na jinsi tunavyoishi katika ulimwengu huu, hatupo nyumbani kwetu.

2 Kor. 5:6-8, "*Basi siku zote tuna moyo mkuu; tena twajua ya kuwa wakati tuwapo hapa katika mwili, tunakaa mbali na Bwana. Maana twaenenda kwa imani si kwa kuona. Lakini tuna moyo mkuu, nasi tunaona ni afadhali kutokuwamo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana.*"

Ni muhimu kwetu sisi kuzingatia kwamba ulimwengu huu sio kwetu.

Tuelewe kwamba sisi tu wasafiri

Msafiri ni mkazi wa muda – mpitaji, mgeni, mhamiaji.

Petro anawaongelea Wakristo kama wahamiaji na wasafiri.

- 1 Pet. 1:1, "*Petro Mtume wa Yesu Kristo kwa Wateule wa Utawanyiko, wakaao hali ya ugenini katika Ponto, na Galatia, na Kapadokia, na Asia, na Bithinia;*"
- 1 Pet. 1:17, "*Na ikiwa mnamwita Baba, yeye ahukumuye kila mtu pasipo upendeleo, enendeni kwa hofu katika wakati wenu wa kukaa hapa kama wageni.*"
- 1 Pet. 2:11, "*Wapenzi nawasii kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tama za mwili zipinganazo na roho.*"

Biblia ina mifano yenye nguvu ya watu wa Mungu wapitaji.

Ibrahimu.

- Mwanzo. 11:31-12:4, "*Tera akamtwaa Abram mwanawe, na Lutu mwana wa Harani, mwana wa mwanawe, na Sarai mkwewe, mke wa Abram mwanawe wakatoka wote katika Uru wa Wakaldayo, waende nchi ya Kanaani, wakafika mpaka Harani wakakaa huko. Siku za Tera zilikuwa miaka mia mbili na mitano; Tera akafa katika Harani. Basi Abram akaenda, kama BWANA alivyomwamuru; Lutu akaenda pamoja naye. Naye Abram alikuwa mtu wa miaka sabini na mitano alipotoka Harani.*"
- Matendo. 7:2-7, "*Naye akasema ndugu zangu na baba zangu, sikilizeni: Mungu wa utukufu alimtokea baba yetu Ibrahimu, alipokuwa katika Mesopotamia, kabla hajakaa Harani, akamwambia, toka katika nchi yako na katika jamaa zako, ukaende hata nchi nitakayokuonyesha. Ndipo alipotoka katika nchi ya Wakaldayo, akakaa Harani, akatoka huko baada ya kufa babaye, Mungu akamhamisha mpaka nchi hii mnayokaa ninyi sasa. Wala hakumpa urithi humu hata kiasi cha kuweka miguu; akaahidi kwamba atampa, iwe milki yake, nay a uzao wake baadaye alipokuwa hana mtoto. Mungu akanena hivi, wazao wake watakuwa wageni katika nchi ya watu wengine, nao watawafanya kuwa watumwa wao, na kuwatenda mabaya kwa muda wa miaka mia nne. Na lile taifa watakaowafanya watumwa nitawahukumu mimi, alisema Mungu na baada ya hayo watatoka, nao wataniabudu mahali hapa.*"
- Ebr. 11:8-10, "*Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako. Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake, akikaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi ile ile. Maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu.*"
- Ebr. 11:13-16, "*Hawa wote wakafa katika Imani, wasijazipokea zile ahadi, bali wakaziona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri kwamba walikuwa wageni na wasafiri juu ya nchi. Maana hao wasemao maneno kama hayo waonyesha wazi kwamba wanatafuta nchi yao wenyewe. Na kama wangaliikumbuka nchi ile waliyotoka wangaliipata nafasi ya kurejea. Lakini sasa waitamani*

nchi iliyo bora, yaani, ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao; maana amewatengenezea mji."

Waisraeli katika Misri.

Mwanzo 15:13-14, "*BWANA akamwambia Abramu ujue hakika ya kwamba uzao wako utakuwa mgeni katika nchi isiyo yake, watawatumikia watu wale, nao watateswa muda wa miaka mia nne. Hata na taifa lile, watakaowatumikia; baadaye watatoka na mali mengi.*"

Israeli katika Babeli.

Zaburi 137:1-6, "*Kando ya mito ya Babeli ndiko tulikoketi, tukalia tulipoikumbuka Sayuni. Katika miti iliyo katikati yake tulivitundika vinubi vyetu. Maana huko waliotuchukua mateka walitaka tuwaimbie; na waliotuonea walitaka furaha; tuimbieni baadhi ya nyimbo za Sayuni. Tuuimbeje wimbo wa BWANA katika nchi ya ugeni? Ee Yerusalemu, nikikusahau wewe, mkono wangu wa kuume na usahau. Ulimi wangu na uungame na kaakaa la kinywa changu, nisipokukumbuka. Nisipoikuza Yerusalemu zaidi ya furaha yangu iliyo kuu.*"

Kukumbuka kwamba ulimwengu huu sio kwetu.

Hatari kuu tunayo kumbana nayo ni kugeuzwa katika ulimwengu huu.

Rumi. 12:2, "*Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.*

Tunaonywa tusiwe kama ulimwengu huu.

- Yak. 4:4, "*Enyi wazinzi hamjui ya kuwa kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu.*"
- 2 Kor. 6:17-7:1, "*Kwa hiyo tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu, nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kuke, asema Bwana Mwenyezi. Basi wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu.*"
- 1 Yoh. 2:15, "*Msiipende dunia wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia kumpenda Baba hakumo ndani yake.*"

Hatupaswi kuwa katika hatua ambayo hatu "sukumwi" na kile tunachokisikia na kukiona.

- Matendo. 17:16, "*Paulo alipokuwa akiwangojea huko Athene na kuona jinsi mji ule ulivyokuwa umejaa sanamu, roho yake ilichukizwa sana ndani yake.*"
- 2 Pet. 2:7-8, "*Akamwokoa Lutu yule mwenye haki, aliyehuzunishwa sana na mwenendo wa ufisadi wa hao wahalifu; maana mtu huyu mwenye haki akikaa kati yao, kwa kuona na kusikia alijitesa roho yake yenye haki, siku baada ya siku, kwa matendo yao yasiyo na sheria;*"

Tunajizuiaje kwa kutokugeuzwa katika ulimwengu huu

Tunapaswa kuwa makini kuhusu tabia zetu.

Kol. 3:1-2, "*Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkno wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi.*"

Tunapaswa kuwa makini na hazina yetu.

Math. 6:19-21, "*Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusipoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako.*"

Tunapaswa kuwa makini na urafiki wetu.

1 Kor. 15: 33, "*Msidanganyike mazungumzo mabaya huaribu tabia njema.*"

Tukikumbuka kwamba mbinguni ndiko nyumbani kwetu

Tunachotakiwa tujitahidi ni "*moyo wa kigeni*".

Kut. 23:9, "*Usimwonee mgeni, maana ninyi mwajua moyo wa mgeni ulivyo kwa kuwa ninyi mlikuwa wageni katika nchi ya Misri.*"

Kwa sababu tuko mbali na nyumbani, lazima tuishi kwa imani.

- 2 Kor. 5:6-8, "*Basi siku zote tuna moyo mkuu; tena twajua ya kuwa, wakati tuwapo hapa katika mwili, tunakaa mbali na Bwana. Maana twaenenda kwa imani, si kwa kuona. Lakini tuna moyo mkuu nasi tunaona ni afadhali kutokuwamo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana.*"

- Ebr. 11:1, "*Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.*"

Tunakuwaje na moyo wa msafiri?

Tunapaswa ku:

- Kusoma na kujifunza kuhusu nyumbani kwetu mbinguni na Baba yetu aliyeko pale.
- Kufikiria kuhusu mbingu.
- Kuzungumza kuhusu mbingu
- Kuimba kuhusu mbingu.

Hitimisho

Fil. 1: 21-23, "*Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida. Ila ikiwa kuishi katika mwili, ni matunda ya kazi; basi nitakalolichagua silitambui. Ninasongwa katikati ya mambo mawili; ninatamani kwenda zangu nikae na Kristo maana ni vizuri zaidi sana.*"